Wapendwa Wazazi na Familia za Carleton,

Karibu kwenye jumuiya ya Carleton! Kama mshirika, una jukumu muhimu na tunatarajia zaidi kushirikiana nawe, mwanafunzi wako anapojiunga na mazingira ya Northfield. Barua hii ni barua ya karatasi ya mwisho unayopaswa kupokea msimu huu wa majira ya kiangazi.

Wiki la Wanafunzi Wapya (maelekezo ya mazingira) imepangwa kuanza tarehe 9 Septemba, 2021. Tembelea **go.carleton.edu/newparents** baadaye katika msimu huu wa majira ya kiangazi ili upate ratiba ya maelekezo ya mazingira kwa wazazi.

Ninakuhimiza pia usome *Mwongozo wa Familia* ambao tumeutayarisha kwa kushirikiana na Kamati yetu ya Ushauri wa Wazazi, ambao umechapishwa pia kwenye ukurasa sawa wa wavuti. Mwongozo huu una maelezo muhimu ambayo mara nyingi huwa mapya kwa wazazi na familia, ikiwa ni pamoja na haki za faragha za wanafunzi, taarifa za wazazi na sera za chuo. Katika chuo cha Carleton, tunashirikiana na wanafunzi kama watu wazima na tungependa kukusaidia ujue mambo unayoweza kutarajia, mwanafunzi wako anapojiunga na jumuiya yetu.

**Ningependa kukualika ujiunge katika mkutano wa mtandaoni kwenye Zoom wa wazazi na familia mpya pamoja nami na Art Rodriguez ’96, Makamu wa Rais na Mshauri wa Mipango ya Usajili wa Wanafunzi na Usaidizi wa Fedha, mnamo tarehe 14 Juni, 2021, saa kumi na mbili kamili jioni (6 pm) CDT (saa moja kamili jioni (7pm) EDT/saa kumi kamili jioni (4pm) PDT)** ili tushiriki maelezo na kujibu maswali yoyote unayoweza kuwa nayo kuhusu chuo cha Carleton, hali ya mwanafunzi, na jinsi Chuo kimejitayarisha kwa na kinavyoshughulikia janga la COVID-19. Utapokea mwaliko kupitia barua pepe wa mkutano huu wa mtandaoni mwishoni mwa mwezi wa Mei, ambao utakuwa na kiungo cha kujisajili (kumbuka kuthibitisha maelezo yako ya mawasiliano katika **go.carleton.edu/newparents**!).

Mimi na wenzangu tunatazamia kumsaidia mwanafunzi wako kupiga hatua na kukua kwa miaka minne ijayo. Asante kwa kutuamini. Iwapo wakati mwingine huna uhakika kuhusu kuwasiliana na mtu katika Chuo ili kuzungumzia suala fulani, tafadhali kuwa huru kuwasiliana.

Tuungane pamoja katika kufanya miaka hii minne ijayo iwe ya mabadiliko ya kweli!

Kila la heri,

Carolyn H. Livingston, Ph.D.
Makamu wa Rais wa Maisha ya Wanafunzi na Mshauri wa Mipango ya Wanafunzi

Wazazi Wapendwa wa Chuo cha Carleton,

Tunafuraha kuwakaribisha nyinyi na wanafunzi wenu kwa Darasa la mwaka wa 2025 la Chuo cha Carleton. Tunaandika ili kujitambulisha na kushiriki njia chache unazoweza kutumia kuwasiliana na jumuiya ya Chuo cha Carleton. Sisi ndio wenyekiti wa sasa wa Kamati ya Ushauri wa Wazazi, kikundi cha wazazi wanaojitolea ili kutoa ushauri kwa Chuo na kuhudumu kama raslimali ya maelezo kwa wazazi wengine. Tunajua kuwa iliwagharimu nyinyi na wanafunzi wenu imani kubwa katika kuchagua Chuo cha Carleton katika nyakati hizi zisizo za kawaida ambapo wengi wenu hamjapata fursa ya kututembelea. Tunatarajia kuwa tutakurahisishia kadri iwezekanavyo hali ya kuwasiliana na kupata maelezo unayohitaji

Kwanza, tunatarajia kuwa utaanza kujifahamisha na Jukwaa la Wazazi/Familia katika **go.carleton.edu/parents**. Jukwaa ni mahali bora zaidi pa kuanzia ukiwa na maswali, kwa sababu tovuti ina viungo vya kuelekeza kwenye ofisi nyingi muhimu za chuo ambazo wewe au mwanafunzi wako atahitaji.  Pia, kuna viungo vya kuelekeza kwa kalenda na taarifa muhimu za chuo, majarida ya wazazi, mikutano ya mtandaoni na mengineyo.

Kwenye Jukwaa utaona pia kiungo cha kuelekeza kwa *Mwongozo wa Familia*, chini ya "Maelezo na Sera." Tunawahimiza wazazi/walezi wote wapya wa wanafunzi wa chuo wasome mwongozo huu, hasa sehemu yenye kichwa cha "Ushauri kwa Wazazi," ambayo ina vidokezo kuhusu mambo ya kutarajia kimaendeleo kadri mtoto wako anavyoendelea katika Chuo cha Carleton. Tafadhali zingatia kwa makini zaidi sehemu ya haki za faragha ya mwanafunzi na taarifa za wazazi.  Chuo kinadhibiti mambo yanayoweza kushirikiwa na wazazi na familia kuhusu wanafunzi wao, kwa hivyo tunawahimiza mfanye mazungumzo muhimu na wanafunzi wenu kuhusiana na matarajio ya makubaliano ya mawasiliano na taarifa kuhusu jinsi wanavyoendelea.

Kupitia kwa Jukwaa, unaweza pia kufikia *Saraka ya Familia* (chini ya "Huduma za Wazazi"), ambayo ina orodha ya mahali ambapo wazazi/walezi wanapatikana, majina na madarasa ya wanafunzi wao na maelezo ya mawasiliano. Tunatarajia kuwa maelezo haya yatakufaa katika kutambua familia nyingine zilizo na wanafunzi katika Chuo cha Carleton katika eneo lako ambazo unaweza kushiriki nazo maelezo, maarifa na mambo yanayokuvutia. Unaweza kufikia saraka iliyosasishwa baada ya tarehe 1 Julai kwa kutumia jina la mtumiaji ambalo ni **parents** na nenosiri **knights2021**.

Ingawa maelezo ya saraka kuhusu wazazi yanazingatiwa kuwa "maelezo yanayopatikana hadharani" katika jumuiya ya Carleton, tunaheshimu faragha ya kila mtu. Iwapo ungependa kubadilisha na/au kuondoa maelezo yako kwenye saraka ya mtandaoni, tafadhali nenda kwa: **apps.carleton.edu/parents/update**.

Ikiwa ungependa kuwasiliana na wazazi/walezi wenzako kwa njia ya barua pepe au mtandaoni:

- Jiunge na kikundi cha barua pepe cha mzazi kwa mzazi katika **apps.carleton.edu/parents/list**
- Omba kujiunga na *Kikundi cha Wazazi cha Chuo cha Carleton* ambacho ni cha faragha na kisicho rasimu kwenye Facebook

Tuna imani kuwa utatambua kwamba chuo cha Carleton ni mazingira yenye usaidizi na elimu ya kina kwa mwanafunzi wako. Ikiwa una maswali au masuala yoyote, tafadhali wasiliana na Ofisi ya

Mshauri wa Mipango ya Wanafunzi kwa (507) 222-4075 au wasiliana na Joe Baggot, Mshauri wa Darasa kwa Wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza katika jbaggot@carleton.edu.

Wako Mwaminifu,

Karen Handelman na Marc Hirshman, Wenyekiti Wenza
Kamati ya Ushauri wa Wazazi ya Chuo cha Carleton
Wazazi wa Abby Hirshman ’20 na Emily Hirshman ‘23